# RC aagiza walimu wanaofanya vizuri wapandishwe vyeo

Na Tiganya Vincent, Tabora

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dkt. Philemon Sengati ameagiza walimu wa shule zinazofanya vizuri katika mitihani ya kitaifa, ndiyo wawe wanateuliwa kuwa Wakuu wa Shule na Maofisa Elimu Kata.

# Serikali kusaka wavuvi haramu popote walipo

Na Ahmad Mmow, Lindi

SERIKALI imesema haitawavumilia wavuvi haramu, badala yake, itawasaka na kuwakamata ili wakutane na mkono wa sheria.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki jana alipokuwa akizungungumza na wavuvi katika Mtaa wa Mchingambili Manispaa ya Lindi.

Waziri Ndaki alisema serikali haitawavumilia wavuvi haramu ambao kwa kiasi kikubwa wanateketeza viumbe vya baharini, maziwa na mito na kuharibu mazingira hivyo itawasaka popote waliko ili sheria ichukue mkondo wake dhidi yao.

"Tutawatafuta na kuwasaka popote walipo, tunawajua. Watapata adhabu kali kwa mujibu wa sheria za nchi," alisisitiza Ndaki.

Alisema japokuwa uvuvi haramu umepungua kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma, lakini vita dhidi ya uvuvi huo lazima iendelee ili kutokomeza kabisa.

Waziri Ndaki alisema, njia pekee ya wavuvi kuepuka mkono wa sheria ni kuachana na uvuvi huo na kuvua kwa kutumia zana za uvuvi zinazokubalika kisheria, badala ya zilizokatazwa kutumika kwa uvuvi.

Ndaki alisema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imejipanga vyema kuboresha sekta ya uvuvi nchini kwa kununua vifaa bora na vya kisasa ikiwemo boti zitakazotumika kwa doria usiku na mchana, ili kudhibiti uvuvi haramu.

Kwa upande wake Katibu wa Umoja Wavuvi Manispaa ya Lindi, Yusufu Jaji alisema umoja huo umewaunganisha na kuwa na sauti moja.

Jaji alisema uwepo wa vikundi shirikikishi vya jamii vya ulinzi wa raslimali za bahari kwa kiasi kikubwa, umechangia kupunguza uvuvi haramu.

Scanned with CamScanner

UHURU

**Sh. milioni 30>> Fed**

DESCMBA 24,2020

# Wafugaji washauriwa kuzalisha ngozi bora na zenye viwango

**RO**

**W**

Na NATHANIEL LIMU, *Singida*

WATAALAMU wa mifugo nchini wamehimizwa kuongeza juhudi katika kuhamasisha na kuelimisha wafugaji umuhimu wa ufugaji bora na wa kisasa, ili pamoja na mambo mengine wazalishe ngozi bora zenye viwango vinavyokidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Wito huo ulitolewa hivi karibuni na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Dk. Stanford Ndibulema, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa ngozi katika kumuingizia kipato mfugaji na taifa kwa ujumla.

Alisema ngozi bora inaanza shambani, hivyo mfugaji anatakiwa ahakikishe inapatikana huku boma la ufugaji likiwa na mazingira mazuri, mifugo inalindwa dhidi ya kupe na ngozi haina alama za ovyo au matundu.

"Mchunagaji awe ni yule aliyepata mafunzo, siyo vinginevyo. Kwa ujumla wataalamu wana wajibu wa kusimamia na kutekeleza mikakati ya kuboresha ngozi. Tukisimamia vizuri uboreshaji wa ngozi, tutawezesha upatikanaji wa nyama bora, ambayo itaingizia mapato ya halmashauri," alisema.

Ofisa Mifugo wa Mkoa wa Mara, Denis Ishengoma, alisema nguvu zaidi ielekezwe katika kutoa elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji ili wabadilike na kuanza kufuga kisasa na kibiashara.

"Halimashauri nazo zitenge bajeti kila mwaka, kwa ajili ya kuhudumia mifugo. Fedha za bajeti zielekezwe kuhudumia mifugo, ikiwemo kutoa chanjo na kuboresha majosho. Kwa njia hiyo, mazao bora ya mifugo yatapatikana na yatakidhi mahitaji," alisema

Aliongeza: "Mkoani Mara, ngozi nyingi zinazalishwa, lakini hazina ubora, hivyo zinaishia kutupwa au kupewa mbwa. Sasa tunapaswa kusimamia na kuhakikisha ngozi zinakuwa bora na zinakidhi viwango vya ndani na nje ya nchi."


Hivi karibuni, washauri wa mifugo mikoani na wataalamu wa wizara hiyo, walifanya kikao kazi mjini Singida, ambacho kilifunguliwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Angelina Lutambi, ambaye alisisitiza ipo fursa kubwa kwa sekta ya mifugo kuchangia pato la mfugaji binafsi na taifa kwa ujumla.

Fursa hizo ni uwepo wa mahitaji ya malighafi za mifugo kwenye viwanda vilivyojengwa sehemu mbalimbali nchini vya kusindika mazao ya mifugo.



Scanned with CamScanner

Uk. 6



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (kulia) akikagua samaki aina ya sato wanaofungwa katika kampuni ya XIN SI LU ya China, iliyopo mkoani Manyara alipofanya ziara mkoani humo juzi. Kulia kwake ni Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Magese Bulayi. (Na Mpigapicha Wetu).

Scanned with CamScanner

# Viongozi wa kata, vijiji waonywa urafiki na wafugaji

**Na Edward Kondela, Liwale**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka baadhi ya viongozi wa vijiji na kata wanaoshirikiana na wafugaji kuvunja sheria, taratibu na kanuni za nchi ili kuwanyanyasa wakulima katika maeneo yao, kuacha mara moja kufanya hivyo kwani viongozi hao wanakuwa wanashiriki katika migogoro kwa kuchonganisha wakulima na wafugaji.

Akizungumza wilayani hapa jana kwenye kikao kilichoshirikisha wakulima na wafugaji wa Mkoa wa Lindi kwa ajili ya kutatua kero zao, Waziri Ndaki alikemea urafiki wa baadhi ya viongozi hao na wafugaji ambao umekuwa ukilenga kuwanyanyasa wakulima, kutokana na wafugaji kuingiza mifugo kwenye maeneo ya wakulima hao.

"Wakati mwingine mnawapa tabu wakulima kwa sababu wafugaji, wanashirikiana na hawa viongozi wetu wa ngazi za chini kufanya mambo yasiyotakiwa sasa tuache, Watendaji wa Vijiji na Kata fuateni sheria, taratibu na kanuni mlizoelekezwa zinazopaswa kuwaelekeza katika kutenda kazi zenu," alisema.

Alifafanua kuwa siku zote, wakulima na wafugaji zimekuwa ni jamii zinazoelewana kwa sababu kila mmoja amekuwa akihitaji huduma kutoka kwa mwenzake kwa maana ya mazao ya kilimo na mifugo na kutaka uhusiano huo, usiharibiwe na baadhi ya viongozi wa ngazi za chini kuingia katikati yao kwa maslahi binafsi na kutaka urafiki usio na tija kwa wakulima kati ya baadhi ya viongozi hao na wafugaji ufe mara moja.

Pia kuhusu sheria, taratibu na kanuni za nchi Waziri huyo alisema nchi haiwezi kuendeshwa kwa sababu jamii moja ya watu wakali na wengine wapole, bali lazima ifuate sheria, taratibu na kanuni zilizopo kutokana na wakulima kulalamikia vitendo vya baadhi ya wafugaji kuwa wakali wanapoingia katika maeneo yao na kulisha mifugo mazao ya wakulima.

"Tukifuata sheria itatusaidia sana kuishi pamoja kama nchi wakulima na wafugaji fuateni sheria, taratibu na kanuni zilizopo ili tuishi pamoja na sheria zimewekwa na wawakilishi wenu Wabunge kwamba wananchi tukiwawekea utaratibu wa namna hii, tunaweza kuishi kwa amani na utaratibu," alisema

Waziri huyo alieleza mkutano huo kati ya wakulima na wafugaji kuwa ni muhimu wafugaji kushirikiana na serikali katika kujenga miundombinu ya ufugaji, yakiwemo malambo ya kunyweshea mifugo yao maji kwenye maeneo ambayo wamekabidhiwa na serikali kufuga mifugo kwa kuwa mahitaji ya wafugaji ni mengi na hayawezi kukamilishwa na serikali pekee kwa mara moja.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaangalia kuanzia bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kujengea malambo katika maeneo mbalimbali nchini kwa kuanzia na baadhi ya vijiji kwa kushirikiana na halmashauri.

Akizungumza kwenye kikao hicho kuhusu ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Ngongo yaliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Waziri Ndaki alisema atazungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo kuingiza bajeti ya awamu ya pili ya ujenzi huo kwa mwaka wa fedha 2021/22 badala ya 2022/23, ambapo ujenzi huo umewekwa sasa unaokadiriwa kugharimu sh. bilioni 2.5.

Waziri huyo aliyatembelea machinjio hayo siku ya kwanza ya ziara yake ya kikazi mkoani humo mwishoni mwa wiki na kushuhudia kukamilika kwa ujenzi wa jengo la machinjio hayo, ambayo yanasubiri awamu ya pili ya ujenzi ya kuweka vifaa vya kuchinjia na kuchakata nyama.

Alisema kwa kuwa jengo la machinjio limekamilika ni vyema likamilike kwa kuwekewa vifaa mapema, ili machinjio hayo yaanze kufanya kazi na kuwanufaisha wafugaji kwa kuwa kwa sasa mikoa ya Kusini, ikiwemo Mikoa ya Lindi na Mtwara imeanza kupokea mifugo mingi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi, hivyo hitaji la mazao ya mifugo litaongezeka na mkoa utaongeza mapato kupitia machinjio hayo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi alisema mkoa umeweka utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji, ambao wamekuwa wakiingia katika mkoa huo, lakini wanakabiliana na gharama kubwa katika upimaji wa maeneo hali iliyolazimu mkoa kusitisha kupokea mifugo kwa sasa kwa kuwa maeneo yaliyotengwa ni machache.

Zambi alisema ni muhimu kuangalia namna ya kudhibiti idadi ya mifugo kutokana na wafugaji kuwa na mifugo mingi, huku wakiendelea kuishi maisha duni na kutaka kuwepo na sheria ya kudhibiti idadi ya mifugo.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki (wa kwanza kushoto) akipatiwa taarifa ya Mkoa wa Lindi na Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi wakati Waziri huyo alipofika katika Wilaya ya Liwale kabla ya kuhudhuria mkutano kati ya wakulima na wafugaji, ikiwa ni siku ya pili ya ziara yake ya kikazi mkoani Lindi.** (Na Mpigapicha Wetu)

## Madiwani Kaliua watakiwa kuiga kasi ya Magufuli

**Na Allan Vicent, Kaliua**

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, wametakiwa kuiga kasi ya utendaji wa Rais Dkt. John Magufuli kwa kutekeleza wajibu wao kwa weledi mkubwa, ili kuharakisha maendeleo ya wananchi wa kata zao.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Katibu Tawala Wilaya ya Kaliua, Michael Nyahinga katika kikao cha kwanza cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo kilichokaa kwa ajili ya kumchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa halmashauri hiyo.

Alisema kasi na weledi wa Rais Magufuli ni kielelezo kizuri kwa kiongozi yeyote yule anayetaka mafanikio, hivyo akawataka madiwani hao kutekeleza wajibu wao kwa wananchi kwa vitendo na si maneno.

Alisisitiza kuwa wananchi wanataka maendeleo na kutatuliwa kero zao na si kuendekeza malumbano yasiyo na tija katika vikao vya baraza, ambavyo ndivyo vyenye mamlaka ya kupitisha mipango ya maendeleo ya wananchi.

"Nawapongeza madiwani wote mlioshinda katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, uchaguzi umeisha sasa kila mmoja akatekeleze wajibu wake kwa kasi, weledi na vitendo na kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria," alisema.

Kwa upande wake Katibu Msaidizi Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Magharibi, Gerald Mwaitebele aliwataka kuzingatia maadili ya utumishi na kujiepusha kumiliki mali za udhalimu, huku akionya kuwa yeyote atakayeenda kinyume na kiapo hicho atachukuliwa hatua za kisheria.

Naye Mwenyekiti mpya wa halmashauri hiyo, ...

Uk. 1, Desemba 24, 2020 MWANANCHI

# MAANDALIZI YA KRISMASI

Mkazi wa jiji la Dar es Salaam (kulia), akichagua mbuzi katika Soko la Vingunguti jana ikiwa ni maandalizi ya Sikukuu ya Krismasi. Mbuzi mmoja sokoni hapo anauzwa kati ya Sh80,000 na Sh120,000. Kushoto ni mchuuzi wa mifugo hiyo, Amani Chuwa. **Picha na Ericky Boniphace**



edaiwa kujinyonga polisi wataka taarifa ya

Scanned with CamScanner

## NIONAVYO

Na Mwandishi Wetu

# Wanaojihusisha na uvuvi haramu tuwafichue

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul amewataka wale wote wanaojihusisha na uvuvi usiozingatia sheria na taratibu kuacha mara moja kwani serikali haitakuwa na huruma kwa watakaokamatwa.

Gekul alitoa onyo hilo alipokuwa akiongea na Wavuvi wa Mkoa wa Manyara alipofanya ziara.

Katika operesheni ya kupambana na uvuvi haramu iliyopita zilitumika karibu sh. bilioni 1. 2, jambo ambalo anasema halivumiliki, na hivyo alitaka wavuvi watoe ushirikiano kwa serikali ili kukomesha vitendo hivyo.

"Hatutavumilia jambo hili liendelee, Sisi kama Wizara tumesema ni lazima tupate muarobaini wa uvuvi haramu lakini na nyinyi wavuvi muwe tayari kutoa ushirikiano kwa serikali ili uvuvi haramu ukomeshwe mara moja," anasema.

Kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikifanya jitihada katika operesheni ya uvuvi haramu jambo ambalo lingekuwa likiporeza fedha nyingi za wananchi kwa kundi dogo lisilofuata sheria.

Imefika wakati sasa kwa kila mmoja kushiriki katika kampeni hiyo kwa kuwafichua wavuvi wanaojihusisa na biashara hiyo haramu.

Mbali na biashara haramu pia wamekuwa wakichangia kupungua kwa samaki ambao wamekuwa wakichangia pato la mwananchi mmoja mmoja na hata Taifa.

Naamini kuwa kama uvuvi haramu utakomeshwa itasaidia kuokoa mazalia ya samaki na kuongeza idadi ya samaki katika maziwa na maeneo mengine.

"Kwa kuwa mmeonesha nia ya kutoa ushirikiano katika hili, shirikianeni na viongozi wenu kuanzia leo hizo nyavu haramu zikatupwe, tusisikie tena kuhusu nyavu haramu iwe mwanzo na mwisho," anasema.

Aidha, Waziri Gekul anasema kuwa kipaumbele cha serikali kwa sasa ni kuimarisha ufugaji wa viumbe maji kwa kutumia Vizimba na Mabwawa jambo ambalo anasema likisimamiwa vizuri litaongeza ajira kwa wananchi na kupunguza umasikini na kuchochea uchumi wa taifa letu.

**Wakati wa operesheni kupambana dhidi ya uvuvi haramu iliyopita zilitumika karibu sh. bilioni 1. 2, jambo ambalo Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi amesema halivumiliki, na hivyo ametaka wavuvi watoe ushirikiano kwa serikali ili kukomesha vitendo hivyo ...**

Ni wakati sasa kwa Wakurugenzi na Viongozi wengine wa Halmashauri kuangalia uwezekano kwenye zile asilimia kumi zinazotolewa na Serikali kwa Vijana, Wanawake na Walemavu badala ya kuwapa mkononi wafanye utafiti ili kujua ujenzi wa mabwawa unagharimu kiasi gani ili wawajengee mabwawa ya kufugia samaki.

Anasema kuwa wakiweza kufanya hivyo watakuwa wamepunguza tatizo la ajira nchini' ambalo lingekuwa changamoto kubwa.

Uvuvi haramu naamini haikubali popote duniani ili kukomesha vitendo hivyo kila Mtanzania ashiriki kwa kuwafichua na kukataa uvuvi haramu nchini.

Gekul anaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa uvuvi kuwafikia wavuvi wote na kuhakikisha wanalipia leseni za uvuvi ili kuzuia upotevu wa mapato na kukuza pato la Serikali nionavyo ni kuwa endapo viongozi hao watasimamia vyema basi uvuvi haramu katika eneo hilo utapungua kama si kumalizika kabisa.

Naamini kama kila atasimamia vizuri kila mmoja atajisikia vizuri kulipa kodi ya serikali ukiwa ni pamoja na kupatiwa risiti za mashine za elekroniki kwa kufanya hivyo kutazuia upotevu wa mapato ya serikali.

Wahakikishe wavuvi wote wanawafikia kwa lengo la kutatua kero zinazowakabili lakini vilevile na kutoa elimu kuhusiana na madhara ya uvuvi haramu.

Pia kuhakikisha kila mmoja anakuwa na leseni ili serikali iweze kuwatambua na kupata mapato kupitia shughuli za uvuvi.

Mwenyekiti wa Wavuvi, Halmashauri ya Babati, Iddi Hassani anasema kuwa watafanyia kazi maelekezo na watahakikisha wanashirikiana na serikali ili wavuvi wote wawe na leseni za uvuvi na wataendelea kupambana na uvuvi haramu ili kunusuru viumbe maji na kuendelea kufanya uvuvi endelevu.

Scanned with CamScanner

# Waziri Ndaki akerwa na viongozi wa vijiji

Mwandishi Wetu, Mwananchi

**Liwale.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewaonya baadhi ya viongozi wa vijiji na kata wanaoshirikiana na wafugaji kuvunja sheria za nchi na kuwanyanyasa wakulima katika maeneo yao.

Ndaki alieleza hayo wilayani hapa Mkoa wa Lindi jana katika kikao kati yake na wakulima na wafugaji ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake mkoani humo kwa ajili ya kutatua kero zinazohusu sekta hiyo.

Ndaki alikemea urafiki wa baadhi ya viongozi hao na wafugaji akisema umekuwa ukilenga kuwanyanyasa wakulima kutokana na wafugaji kuingiza mifugo kwenye maeneo ya wakulima.

"Wakati mwingine mnawapa tabu wakulima kwa sababu wafugaji wanashirikiana na hawa viongozi wetu wa ngazi za chini kufanya mambo yasiyotakiwa sasa tuache, watendaji wa vijiji na kata fuateni sheria, taratibu na kanuni mlizoelekezwa zinazopaswa kuwaelekeza katika kutenda kazi zenu." alisema Ndaki.

Ndaki alisema siku zote wakulima na wafugaji zimekuwa jamii zinazoelewana kwa sababu kila mmoja amekuwa akihitaji huduma kutoka kwa mwenzake.

"Tukifuata sheria itatusaidia sana kuishi pamoja kama nchi wakulima na wafugaji fuateni sheria, taratibu na kanuni zilizopo ili tuishi pamoja, na sheria zimewekwa na wawakilishi wenu wabunge kwamba wananchi tukiwawekea utaratibu wa namna hii tunaweza kuishi kwa amani na utaratibu." alisema Ndaki

Mkuu wa Mkoa wa Lindi Godfrey Zambi alisema wameweka utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji ambao wamekuwa wakiingia katika mkoa huo, lakini wanakabiliana na gharama kubwa katika upimaji wa maeneo.

"Kwa sasa tusipokee tena mifugo kwa sababu hatuna pa kuiweka, ardhi tunayo lakini hatuna sehemu tulizopima, hivyo ikija inakuwa vurugu na kukaribisha ugomvi kati ya wafugaji na wakulima," alisema Zambi.

Scanned with CamScanner

 MWANANCHI, 24/12/2020

# *Gekul: Marufuku biashara ya punda

Joseph Lyimo, Mwananchi
jlyimo@mwananchi.co.tz

**Babati**. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul amepiga marufuku biashara ya punda ili kuruhusu wanyama kazi hao kuongezeka nchini baada ya kasi ya kuwachinja kuwa kubwa.

Gekul ambaye pia ni mbunge wa Babati Mjini alieleza hayo jana kwenye kikao cha ushauri cha Mkoa wa Manyara kilichofanyika mjini Babati.

Alisema watu wanaofanya biashara hiyo waache mara moja kwani idadi ya punda nchi nzima inazidi kupungua na hivi sasa wamefikia 600,000.

Alisema kupitia wizara yake watawasiliana na viwanda ambavyo vimekuwa vikifanya biashara ya kuchinja punda ili viache kuwaua wanyama hao.

"Wanaofanya biashara hii waache mara moja, tukisema biashara hii iendelee maana yake mama zetu wabebe ndoo za maji kichwani," alisema.

Alisema hawatakubali biashara hiyo kuendelea kwa kuwa nchi itapoteza wanyama kazi hao ikiwa wataendelea kuuzwa na kuchinjwa.

Desemba 12, mwaka huu wadau wa sekta ya mifugo nchini walisema endapo Serikali isipoingilia kati kuratibu biashara ya nyama ya punda, miaka michache ijayo wanyama hao watatoweka kabisa nchini.

Wakizungumza katika kikao cha wadau wa Sekta ya Mifugo jijini Arusha, baadhi ya washiriki walieleza punda wamekuwa wakinunuliwa vijijini kwa wingi na hivyo kupunguza nguvu kazi ya kilimo, kusafirisha maji na mizigo.

Mkurugenzi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii Afrika (Inades), Herman Hishamu alibainisha kuwa idadi ya punda nchini ni takriban 660,000 na kwamba mnyama huyo hutumika zaidi na watu wenye kipato cha chini kwa ajili ya kulima na kubeba mizigo.

Siku hiyo Gekul aliahidi kuanza kufuatilia kupotea kwa wanyama hao kutokana na ongezeko la viwanda vya kuwachinja, jambo ambalo amelitekeleza kwa kuzuia biashara ya punda.

Katika hatua nyingine, Gekul alisema wataanza msako wa wafugaji ambao hawachinji mifugo yao.

Alibainisha kuwa licha ya Serikali kufanya misako ya wavuvi haramu, awamu iliyopita ilitumia zaidi ya Sh1.2 bilioni kufanya operesheni za kuzuia uvuvi haramu.

Aliwapongeza wavuvi 1,500 wanaovua samaki katika Ziwa Babati ambao aliongea nao wakakiri kuwa walikuwa hawana leseni na hivi sasa wataenda kukata leseni ili walipe kodi ya Serikali.

> 'Wanaofanya biashara hii waache mara moja, tukisema biashara hii iendelee maana yake mama zetu wabebe ndoo za maji kichwani.'
>
> Pauline Gekul

*

Scanned with CamScanner

The Guardian Pg. 5

# * Govt announces new sustainable crackdown on unlawful fishing *

By Guardian Reporter

THE government has announced a crackdown on fishermen engaged in illegal fishing, warning that this time the operation will be sustainable.

It says the crackdown would aim at all those engaged in illegal fishing practices wherever they might be and stern legal steps would be taken against them.

Mashimba Ndaki, the Livestock and Fisheries Minister made the announcement at a public rally at Mchinga 2 Village in Mchinga District in Lindi Region during his tour in the region.

He said the operation would be inclusive in all regions and districts with known illegal fishing activities.

"We want this operation to be sustainable, we want to completely eradicate illegal fishing practices which we think will now remain in history books," Ndaki said.

He added: "I warn all those engaged in illegal fishing, or those contemplating doing so, to start thinking doing other things because we shall have no mercy at all, we shall hunt for them everywhere and ensure they face the arm of the law."

He said despite huge government efforts against illegal fishing, the crimes still continue and that the government would not tolerate them anymore.

He also said there was need for the people in areas with illegal fishing activities to work together with the government in eradicating them.

"I congratulate the people living along the Indian Ocean Coastal areas for exhibiting patriotism by working together with the government in fighting illegal fishing, especially dynamite fishing, and according to reports Lindi Region has controlled the crime by 100 per cent within this particular area," he said.

Ndaki called on firms which purchase seaweeds crop to immediately stop swindling seaweed farmers by using defective weighing scales.

He said his ministry will look into the procedures by working together with local councils to enable seaweed farmers add value to their crops instead of selling them as mere raw materials.

He said the time has come for farmers to benefit from their crops instead of being swindled by some middlemen.

**"We want this operation to be sustainable, we want to completely eradicate illegal fishing practices which we think will now remain in history books**

Pg. 1, THE GUARDIAN, 24/12/2020

# Govt restores ban on donkey selling

By Guardian Correspondent, Babati



THE government has banned selling donkeys in a fresh move to boost the number of the domestic animals, lately threatened by high demand in China for traditional medicine called 'ejiao.'

Pauline Gekul (pictured), the Deputy Minister for Livestock and Fisheries announced the ban here on Tuesday when addressing the Manyara Regional Consultative Committee (RCC).

The trade is wreaking havoc on rural economies that depend on donkeys for transport, she said, highlighting that donkey skins are used to make gelatin–a key ingredient of 'ejiao,' which is believed to improve blood circulation and treat conditions like anaemia, by precepts of Chinese traditional medicine.

The deputy minister asked people currently involved in donkey slaughter to find other occupations or engage in the cattle meat trade, elaborating that the number of donkeys in the country is estimated at

TURN TO PAGE 2

Scanned with CamScanner

The Guardian Pg. 2

# Ministry: Crackdown on foreign teachers coming

FROM PAGE 1

to provision of education in secondary schools and wider.

Prof Ndalichako said that she was in consultations with the Minister of State (PMO) for the portfolio, Jenister Mhagama to ensure the crackdown starts shortly. "We are not going to spare anyone; stringent measures will be taken against them," the minister underlined.

She urged secondary school heads to ensure proper supervision of the country's laws and report to the government whenever school owners bring foreign teachers without following the laid down procedures.

Measures against illegally employed teachers are meant to protect jobs for locals but also ensure schools, colleges and universities respect the country laws, she asserted, cautioning school owners against violating the terms of registration for their schools.

"Some owners have been turning their day schools to boarding schools simply because they have just constructed one or two structures and call them dormitories; this is unacceptable," said Prof Ndalichako insisting that they follow procedures to be granted permits to operate boarding schools.

She urged the school heads to make sure students are well taught throughout the year instead of waiting for national examinations to start teaching them after normal class hours.

The Tanzania Association of Managers and Owners of Non-Government Schools and Colleges (Tamongsco), colleges in the country says that there aren't enough trained primary school tutors who focused on English studies.

It says in a [illegible]

December 2015, 3,500 teachers from Kenya, Uganda, Malawi and Zambia faced expulsion in a crackdown on illegal immigrants in the country, on account of the fact that schools are required to pay a $2,000 fee for a two-year work permit required for foreign teachers.

Mwita Waitara, the Deputy Minister of State in the President's Office (Regional Administration and Local Governments), told the National Assembly last year that 3,089 expatriate primary school teachers were employed in the financial year that ended June 2019.

These additional teachers were still inadequate to meet the required teacher-pupil ratio of 1:40 as in some regions, one teacher handles up to 250 students, he added.

**"Some owners have been turning their day schools to boarding schools simply because they have just constructed one or two structures and call them dormitories; this is unacceptable**

Scanned with CamScanner

THE GUARDIAN Pg. 1

THURSDAY 24 DECEMBER, 2020

# National Pg 5

## Govt crackdown on illegal fishing



Scanned with CamScanner



**WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akizungumza wakati wa kikao cha wakulima na wafugaji Mkoa wa Lindi, wilayani Liwale, jana.** (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

# Watafiti wabaini mikunde huongeza kiwango cha maziwa kwa wanyama

**Na DEVOTHA SONGORWA,** *Dodoma*

TAASISI ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Kituo cha Mpwapwa (TALIRI), imebainisha kuwa ng'ombe aina ya Mpwapwa, wana uwezo wa kutoa maziwa lita tano mpaka lita 10, ambazo ni zaidi ya mara nne ya maziwa anayoyatoa ng'ombe wa asili.

Hayo yalibainishwa jana, wilayani Mpwapwa, jijini Dodoma na Kaimu Mkurugenzi TALIRI, Dk. Aluna Chawala na kuongeza kuwa, ulishaji wa mchanganyiko wa mikunde, huongeza kiwango kikubwa cha uzalishaji wa maziwa na nyama.

Alisema vipo vikwazo vinavyokabili sekta ya mifugo, ikiwemo aina ya mifugo na mifumo ya uzalishaji, magonjwa ya mifugo, malisho sahihi na baadhi ya wafugaji kutokuwa na elimu ya ufugaji.

"Kupatikana kwa ngo'mbe aina ya Mpwapwa, ambaye ni mchanganyiko wa ng'ombe wa asili na wa bara la Asia, ni suala la kujivunia na ni wa maziwa na nyama, tukasema tupate mwenye nyama nyingi, lakini awe na maziwa kiasi," alisema Dk.Chawala.

Alieleza kuwa ng'ombe aina ya Mpwapwa, anaweza kuzalisha lita 3,000, kwa kipindi cha ukamuaji wake, sawa na wastani wa lita 10 hadi 16, kwa siku, kutegemea atakavyotunzwa.

"Hii teknolojia tunawasambazia wafugaji kuwajengea uelewa, ana sifa ya kuishi kulingana na mazingira na tuna majike na madume. Kwa majike ni kuzalishia, lakini madume ndiyo tunasambaza zaidi ili kuongeza wingi wao," alieleza.

Akizungumzia lengo la kuwepo kwa teknolojia hiyo, Mtafiti Idara ya Ng'ombe, Deogratius Masao, alibainisha kuwa teknolojia ya kuzalisha ng'ombe chotara ni kuboresha mifugo asili na kuwajengea wafugaji mazingira bora ili wajipatie kipato kizuri .

Mtafiti Idara ya Mbuzi, Boniface Paschal, alifafanua kuwa mbuzi aina ya Malya au Blended, ni aliyetokana na utafiti uliokusudia kuzalisha mbuzi anayefaa kwa nyama na maziwa.

"Wametengenzwa kuhimili mazingira kama magonjwa, malisho hata uzito wa nyama, ambao unafika mpaka kilo 30. Wako mbuzi wa asili, lakini

wameboreshwa na kuna uhitaji mkubwa wa maziwa ya mbuzi. Tumepata oda nyingi sana, na wanazaa mapacha hadi watatu, tunaishukuru serikali kwa kutuunga mkono," alisema.

Alhamisi Desemba 24, 2020 Uhuru.